Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.361
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 13.02.2022; Accepted 16.02.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kiguta, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

ISSN: 2663-9289

# Maudhui Yaliyotumiwa katika Utunzi wa Michezo ya Kuigiza kuhusu Ukimwi Katika Mashindano ya Sanaa za Shule za Upili.

Michael Kiguta.
Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.
Email: mchlkiguta@yahoo.com

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kutambua maudhui yaliyotumiwa katika utunzi wa michezo ya kuigiza kuhusu ukimwi katika mashindano ya sanaa za shule za upili. Maeneo ya utafiti yalitokana na uchunguzi wa michezo miwili, ambayo ilikuwa: *Chozi* (2001) na *Majuto* (2001). Tulitumia michezo kama sampuli iliyowakilisha michezo yote ya Kiswahili iliyokuwa na mada kuhusu ukimwi. Uteuzi ulitokana na sababu kuwa ulihusu vipengele vya kimsingi kama vile: uhusika, mandhari, jukwaa, kitendo, ploti, lugha maleba na jumuiya. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktabani ulitumia hadhira tuli ya kimaandishi. Data zilizokusanywa kutoka nakala za michezo ziliainishwa kupitia vigezo mbalimbali vya matumizi ya maudhui. Makala hii ilibaini kuwa watunzi walitumia maudhui mbalimbali kukuza mada ya ukimwi. Baadhi ya maudhui ambayo yalitumiwa yalikuwa ya: mila na utamaduni, uhafidhina, asasi za ndoa, utabaka, utamauushi, uana, malezi, ufuska, uzinzi na kadhalika. Maudhui ulitumiwa kubeba ujumbe kuhusu ukimwi. Utafiti huu ulipendekeza kuwa maudhui yaliyojadiliwa yangefaa kuwa katika tajriba ya vijana ya kila siku, maudhui ya ukimwi yangelijadiliwa bila kutumia mbinu ya kitanzia, ingekuwa bora kama tamthilia zingelijadili jinsi ya kuishi na waathiriwa wa ukimwi badala ya kuwatenga kama ilivyokuwa katika tamthilia ya *Majuto,* tamthilia ingetumika kwa njia ya ushawishi kuhusu ugonjwa wa ukimwi badala ya kulaumu na kukemea, mtunzi angeonyesha kuwa maafa si suluhu la matatizo bali ni kutorokea hali ngumu kwa njia ya kifantasia, ingekuwa bora kwa mtunzi kumuondoa katika tamthilia nzima kwa kuwa alifanaya kazi ya mtunzi iwe na udhaifu kisha kulihitajika watunzi wengi wa shule za upili wajitokeze ili tamthilia itumike vilivyo kama chombo mahsusi cha upashanaji wa ujumbe dhidi ya ukimwi.

**Maneno muhimu:** michezo ya kuigiza, ukimwi, Sanaa, shule za upili.

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA.**

Kiguta, M. (2022). Maudhui Yaliyotumiwa katika Utunzi wa Michezo ya Kuigiza kuhusu Ukimwi Katika Mashindano ya Sanaa za Shule za Upili. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 4(1), 422-426. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.361

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.361
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
ISSN: 2663-9289
Received: 13.02.2022; Accepted 16.02.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kiguta, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## UTANGULIZI

Ukimwi ni miongoni mwa majanga makubwa katika taifa la Kenya. Ni tisho lililo kubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na ukweli kwamba suluhisho bado halijapatikana. Mnamo mwaka wa 1999, Serekali ya Kenya ilitangaza kuwa ukimwi ni janga la taifa. Malengo makuu ya sera ya taifa yalizindua vyombo mbalimbali, miradi na mikakati ya kupambana na maenezi ya ugonjwa huu. Kwa kuwa swala la ukimwi limeendelea kuwa sugu na la kutia hofu katika jamii, utafiti huu ulichunguza utanzu wa tamthilia kama mojawapo ya chombo kilichotumiwa kuhamasisha na kuizindua jamii kuhusu ugonjwa huu. Utafiti ulichunguza vipengele vilivyojenga tamthilia na kuvihakiki. Utafiti wa kuhakiki tamthilia kama nyenzo ya uhamasishaji umma dhidi ya ukimwi, ulikuwa bado haujulikani.

Michezo ya kuigiza bali na kuwatumbuiza wanafunzi kila mwaka, huwapa wanafunzi nafasi ya kuigiza mbele ya hadhira. Wanafunzi hushiriki katika sifa msingi za kisanaa ambazo ni kutumbuiza, kuelimisha na kuburudisha hadhira, na wao wenyewe. Kupitia uigizaji, hukuza ukwasi wao wa lugha, mbinu za ubunifu, mbinu za mawasiliano na kuwa wakakamavu. Kwa njia wanafunzi hujifunza taaluma ya maigizo ya siku za usoni. Maswala ibuka wanayojadili kupitia maigizo huwafikia walengwa wao kupitia mbinu hizi za kimaigizo. Kwa hivyo, makala hii imetambua maudhui yaliyotumiwa katika utunzi wa michezo ya kuigiza kuhusu ukimwi katika mashindano ya sanaa za shule za upili.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Kwa mujibu wa Abrahams (1999), wazo kuu lilikitwa kwenye hadithi. Aghalabu ujumbe ulihusu hali za maisha ya jamii. Maudhui yaliibuka kutokana na muoano wa ploti, wahusika, mielekeo ambayo mtunzi alizingatia, na hadithi. Wamitila (2003) alifafanua dhana ya maudhui kwa kuilezea kwa a jumla ya mambo yote yaliyozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Maudhui yalitumiwa kwa upana kujumlisha vitengo mbalimbali vya fasihi kama vile dhamira, falsafa, itikadi na msimamo wa mtunzi.

Mule (1991) alitafiti utanzu wa tamthilia na kushughulikia swala la nafasi ya mwanamke katika jamii. Alichunguza maudhui ya swala la mwanamke kama yalivyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa kike katika nchi ya kenya na Tanzania. Mule alishughulikia uchanganuzi wa matini ya kimaandishi. Maudhui yaliyotawala utafiti wake yaliegemea upande wa swala la ukombozi wa wanawake. Kupitia utafiti wake, wanawake walikuwa wamedunishwa katika jamii. Mule alitumia nadharia ya kifeministi na jinsia kuchunguza jinsi wanawake walivyochorwa na waandishi kama vyombo vya anasa na starehe. Mkabala aliochukua ulikuwa wa ubaguzi dhidi ya wanawake. Utafiti wetu ulichunguza mbinu za kisanaa zilizotumiwa katika uhamasishaji wa ugonjwa wa ukimwi katika shule za upili. Ndungo (1985) alishughulikia swala la mwanamke kupitia mashairi ya Binti Saad. Alijikita pia kwa maswala ya wanawake na jinsi walivyobadilika kihistoria. Madhumuni ya utafiti wa Ndungo ulitofautiana na wetu kwa kuwa alishughulikia utanzu wa ushairi, ilihali utafiti wetu ulijikita katika utambuzi wa maudhui katika tamthilia.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Maudhui katika Tamthilia za Shule za Upili

Kupitia madhumuni ya utafiti wetu, matokeo yalionyesha kuwa tamthilia za shule za upili zilitumia maudhui mbali mbali. Tamthilia ya *Chozi* ilibainisha na kunakili maudhui yafuatayo: mila na utamaduni, utasa, ukimwi, ufuska, ndoa na mapenzi, uzinzi, ukandamizaji, tamaa, uhafidhina, nafasi ya mwanamke na taasubi za wanaumme, umbeya, usaliti, unafiki, uavyaji mimba na urithi. Tamthilia ya *Majuto,* ilituwezesha kuorodhesha maudhui yafuatayo: majuto, ukimwi, unyanyapa, ndoa, utabaka, utamaushi, uhafidhina, ukatili, nafasi ya mwanamke taasubi ya wanaumme na malezi. Kulikuwa na jumla ya maudhui tisa (9), yaliyonakiliwa. Hii ilithibitisha kuwa watunzi waliweza kutumia maudhui mbalimbali katika ujenzi wa tamthila zao. Katika tamthilia ya *Chozi* kulikuwa na maudhui kumi na mbili



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.361
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 13.02.2022; Accepted 16.02.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kiguta, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

(17). Kupitia madhumuni ya utafiti, matokeo ya data yalionyesha kuwa watunzi watumia maudhui mbalimbali katika ujenzi wa tamthilia.

Swala la ukimwi lilijadiliwa kwa mapana na marefu katika tamthilia za shule. Mtunzi wa *Majuto* alimtumia mhusika Majuto kama kielelezo cha vijana waliaoathiriwa na ukimwi. Majuto aliambukizwa na ukimwi baada ya tendo la ubakaji alipobakwa safarini na majambazi ambao waliosimamaisha gari walimokuwa wakisafiria. Babake Majuto aliyekuwa afisa katika Wizara ya Afya hakutaka kusikia kuwa mwanaye angeliambukizwa na ugonjwa huu ulioambatanishwa na ufuska. Hakutaka kunasibishwa na gonjwa ambalo lingelimletea kashfa kazini.Kazi aliyoienzi na kuitumikia kama Waziri. Mielekeo hasi iliyochukuliwa na jamii, ilimpa msukumo wa kumfukuzilia mbali mwanawe. Alikataa kuhusishwa na tendo la mwanawe na kumtema. Jambo hili lilimfanya Majuto atamauke na maisha na kufikia uamuzi wa kujitia kitanzi. Mtunzi alitumia mbinu ya tamthilia tatizo ya kisaikolojia kuonyesha jinsi maudhui ya ukimwi yalivyoweza kutatiza jamii pindi mtu alipokuwa amembukizwa na ukimwi. Jamii ilimchukulia mgonjwa wa ukimwi kama mtendaji maovu aliyepasa kulaaniwa.

Katika tamthilia ya *Chozi,* maudhui ya ukimwi yalishughulikiwa kutokana na shauku ya kumpata mtoto. Msukumo wa jamii kuhusu utasa ulimchukulia mwanadamu kama kiumbe kilichokuwa na udhaifu. Simba Wanga alimshurutisha mkewe Tatu amzalie mtoto ambaye angerithi mali yake. Kwa kuwa Tatu alikuwa tasa, kutokana na sababu za kitambo zilizomfanya afungwe mimba alipoavya mimba, alienda kujamiiana na shogake wa zamani kwa jina Kosa. Tamaa na mshawasha ya kumpata mtoto ilimletea mashaka alipojipata ameambukizwa na virusi vya ukimwi. Simba Wanga na Tatu walipokuja kufahamu haya walijutia walipogundua kifo kiliwakodolea macho.

Tamthilia za shule za upili zilishughulikia maudhui ya mila na desturi. Mielekeo hasi ya jamii kupitia tamaduni zilizopitwa na wakati zilishughulikiwa. Katika jumuiya ya *Chozi,* jamii iliendeleza maudhui ya uzazi na ubabe dume. Mwanamume gumba alikashifiwa na kusimangwa, jambo lilomfanya Simba Wanga kutafuta mtoto kwa udi na uvumba ili atosheleze mahitaji ya jamii. Ukosefu wa kizazi ulichukuliwa kama upungufu na udhaifu wa uwezo kujamiiana. Mwanamume aliweza kujisifia nguvu yake kwa uwezo wa kupata mtoto. Ilikuwa ni desturi ya jamii kuwa mzazi angepata mrithi wa mali ya baba mzazi. Tokeo la kuwa Simba Wanga alikuwa mgumba kutokana na ripoti ya daktari lilikuwa pigo kubwa maishani mwake. Alivunjika moyo na kutosadiki kuwa aliyekuwa mgumba. Alimshinikizia mkewe Tatu kwa kutompatia mrithi. Chuki na hasira alizielekeza kwa mkewe hata kuamua kumtaliki. Kwa kuogopa kutalikiwa na mumewe pamoja na simango za jamii kama mwanamke aliyeshindwa kuzaa, Tatu alimwendea Kosa na kujamiiiana naye ili amtoshlezze mumewe na jamii kuwa angeliweza kupata mtoto.

Maudhui ya utasa, urithi, ubabe dume, na uzazi yalitumiwa katika tamthilia hii. Maudhui haya yalionyesha jinsi watu walivyojaribu kujikomboa kutokana na tamaduni zilizopitwa na wakati na matatizo waliyokumbana nayo. Katika *Majuto,* ugonjwa wa ukimwi ulinasibishwa na tabia za kizinzi. Mwelekeo hasi wa jamii ulimpelekea Babake Majuto kumfukuzilia mbali mwanawe ili aridhishe matakwa ya jamii. Matarajio ya jamii yalifanya mzazi kutengana na mwanawe ili kukwepa fedheha iliyowekwa na jamii. Maudhui ya unyanyapa na ukatili yalifungamana na maudhui haya ya utamaduni na mila za jamii.

Taasubi ya kiume ni maudhui yaliyojadiliwa katika tamthilia za *Chozi* na *Majuto*. Mtunzi wa *Chozi* alimtumia mhusika mkuu Simba Wanga kama kielelezo cha mfumo wa ubabe dume. Mtunzi alionyesha mfumo uliowabagua wanawake kama viumbe duni ambavyo kazi yao ni ilikuwa ni kuzaa. Mkewe Tatu hakupewa nafasi yoyote kuongea mbele ya mumewe kuhusu maswala ya uzazi. Mumewe ndiye aliyekuwa muamuzi wa kila jambo. Alitishwa kutalikiwakama hangelimzalia mrithi wa mali yake. Nafasi ya mwanamke haikutambuliwa katika *Chozi.*



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.361
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 13.02.2022; Accepted 16.02.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kiguta, M., *Editon Cons. J. Kiswahili*. Double –Blind Peer Reviewed Journal

Katika *Majuto,* mwanamke hakupewa nafasi ya kutoa maoni mbele ya mumewe. Wanawake hawakusikilzwa. Jamii ilipitia mfumo wa taasubi za kiume.Kama ilivyo katika *Chozi,* babake Majuto alitishia kumtaliki mkewe na kumfukuzilia mbali kwa kuwa mwanawe aliambukizwa na ukimwi. Katika jumuiya hizi, wanaumme walitumia nyenzo za kuwadhalilisha wanawake wao.

Maudhui ya tamaa yaliendelezwa katika *Chozi* na mhusika Tatu. Tamaa ya uzinzi na anasa zilimtawala Tatu alipokuwa bado banati shuleni. Alitembelea vilabuni, kucheza densi na kutumia vileo. Matokeo yake ilikuwa ni kuavya mimba. Hii ilimletea utasa katika ndoa yake. Tamaa ya kumpata mtoto ilishinikiwa na mumewe na jamii ilimfanya amwendee rafikiye wa zamani, Kosa, wajamiiane naye. Tamaa hii ilimuongoza kaburini kwa kuwa Kosa alimbuambukizwa ukimwi. Maudhui ya tamaa na anasa zilioana vizuri na matokeo ya ukimwi. Simba Wanga alikuwa na tamaa ya kupata mtoto ambaye angerithi mali yake. Alikwenda kumuona muuguzi kwa hamu na matarajio makubwa ili apate chanzo cha kutopata mtoto. Jawabu alilopewa lilimuatua moyo. Kiini cha kutompata mtoto ni kuwa alikuwa mgumba. Matarajio makubwa ya jamii kuhusu kumpata mrithi zilichangia pakubwa katika msukumo wa tamaa aliyokuwa nayo Simba wanga.

Majuto ni maudhui mengine yaliyojadiliwa na watunzi wa tamthilia hizi. Katika tamthilia ya *Majuto*, maudhui haya yalijitokeza pale ambapo babake Majuto alipojuta kwa kumfukuzilia mbali mwanawe baada ya kung'amua kuwa hakuwa mkosaji. Alimuomba msamaha pamoja na aila yake aliyoitenga. Alimtaka mwanawe arudi nyumbani na aepuke na wazo la kujitia kitanzi. Alijutia tendo lake la kutomsikiliza mkewe na jinsi alivyoidunisha familia ya baba Dora huku akijisifu na kujigamba kuwa ilikuwa ya watu wachochole na masikini. Katika tamthilia ya *Chozi,* maudhui ya majuto yalijitokeza wakati Simba Wanga alijutia kwa kumshurutisha mkewe kupata mtoto kama mrithi wa mali yake. Tatu alijutia kujiingiza katika shimo la uasherati kwa malengo ya kumpata mtoto ambaye angelifurahisha roho ya mumewe. Wahusika wote wawili walijaa fadhaiko na masikitiko walipogundua kuwa malengo yao yaliangulia patupu. Badala ya kupata mtoto walitumbukia katika dimbwi la ukimwi.

Nafasi ya mwanamke ni maudhui yaliyojadiliwa kwa kina na watunzi wa tamthilia za shule. Mwanamke alitumiwa kama kifaa cha kumridhisha mwanamume. Maudhui haya yalijitokeza kupitia wahusika Dora katika *Majuto* na Tatu katika *Chozi.* Bali na kuwa wanawake hawa walipenda uzinzi walitumiwa na wanaumme kama vyombo vya anasa. Tatu alifanya mapenzi na Kosa mpenziye wa zamani ili wapate mtoto. Vilevile, uzinzi ndiyo uliomfanya Tatu kuavya mimba alipokuwa kijana. Vijana wanaumme walimwandama Dora na kumfanya akosane na mamaye.

Mwanamke aliwasilishwa na watunzi kama kiumbe cha kuzaa, kulea na kufanya kazi za nyumbani. Simba Wanga alimtaka mkewe amzalie mtoto ili afidie matakwa ya jamii. Mwanamke hakupewa mamlaka katika jamii. Alipewa kazi za kiwango cha chini ikilinganishwa na mwanamume. Kazi za wanawake zilikuwa za katibu katika wizara ya Afya na wafanyakazi nyumbani.

Maudhui ya ndoa yalionyesha mahusiano yaliyopo kati ya mume na mke. Wanawake walichukuliwa kuwa chini ya wanaumme zao. Walichukuliwa kama viumbe dhaifu. Ndoa ziliingia doa iwapo pangelitokea msukosuko katika maisha yao. Wakati Simba Wanga alipokosa mtoto wa kumrithi, alimlaumu mkewe. Katika kilele cha mateso yote, mwanamke ndiye alipokea kipigo kikubwa kutokana na kutukanwa na kutalikiwa na mumewe. Mwanamke hakuwa na uwezo wa kumwacha mumewe bali uamuzi wote ulitoka kwa mumewe. Lawama nyingi za kutompata mtoto kutoka kwa mumewe simba Wanga zilimfanya Tatu asumbuke kisaikolojia na simanzi katika ndoa yake. Hili lilimshurutisha atafute njia ya kujikomboa na kupata mtoto, hata ingawa mumewe pia alikuwa mgumba.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.361
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 13.02.2022; Accepted 16.02.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kiguta, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Kwa upande mwingine, babake Majuto alimlaumu mkewe hata kumfukuzilia mbali atokomee na mwanawe popote ambapo angelienda. Katika *Majuto,* wanawake hawakupewa nafasi mbele ya waumme zao. Maoni ya mamake Majuto yalipuziliwa mbali na mumewe kuhusu mwanawe Majuto. Asasi ya ndoa katika tamthilia hizi ilichukuliwa kama nyenzo ya kumdhalilisha mwanamke.

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Watunzi walitumia maudhui mbalimbali kukuza mada ya ukimwi. Baadhi ya maudhui ambayo yalitumiwa yalikuwa ya: mila na utamaduni, uhafidhina, asasi za ndoa, utabaka, utamauushi, uana, malezi, ufuska, uzinzi na kadhalika. Maudhui ulitumiwa kubeba ujumbe kuhusu ukimwi.

**Mapendekezo:** Maudhui yaliyojadiliwa yangefaa kuwa katika tajriba ya vijana ya kila siku. Baadhi ya maudhui yaliyojadiliwa yalikuwa ya kiwango cha juu kupita hali ya vijana ya kila siku. Maudhui ya ukimwi yangelijadiliwa bila kutumia mbinu ya kitanzia. Ingekuwa bora kama tamthilia zingelijadili jinsi ya kuishi na waathiriwa wa ukimwi badala ya kuwatenga kama ilivyokuwa katika tamthilia ya *Majuto.* Ingekuwa bora vilevile kutumia tamthilia kwa njia ya ushawishi kuhusu ugonjwa wa ukimwi badala ya kulaumu na kukemea.

Kulikuwa na tamthilia chache mno za lugha ya Kiswahili ilhali Kiswahili ndiyo lugha ya taifa iliyo na wazungumzaji wengi na iliyofaa zaidi katika kupashia ujumbe muhimu kuhusu maswala ya ukimwi. Kulihitajika watunzi wengi wa shule za upili wajitokeze ili tamthilia itumike vilivyo kama chombo mahsusi cha upashanaji wa ujumbe dhidi ya ukimwi. Ni kwa njia hii ndivyo ujumbe huu ungeliweza kuwafikia vijana wengi kwa kuwa hao ndio walio katika hatari ya maambukizi.

## MAREJELEO

Abrahams, M. (1999). *Glossary of Literary Terms*. USA: Harcourt Brace College Publishers.
Mule, K. (1981). *Swala La Mwanamke Katika Tamthilia Za Kiswahili: Waandishi wa Kike Katika Njia Panda* Tasnifu ya MA, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.
Ndungo, C. M. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria.* Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya M.A.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi-Istilahi na Nadharia*. Focus Publications Ltd.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org